# LEARNING BY EAR

## Lent luxury – The risks of raising credit.

## EPISODE TWO: THE DISCOMFORT OF LIVING IN DEBT

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**<u>LIST OF CHARACTERS BY SCENE</u>**

**<u>SCENE ONE: JD SKIVES OFF CLASS</u>**

- **TEACHER MANDO (F 30)**
- **GIDDY (M 15)**
- **JENNY (M 15)**
- **WINNIE (F16)**
- **YOUNG CROWD (min. 6, c. 15 years old, mixed gender)**

- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE TWO: AT GIDDY'S.</u>**

- **JD (M 15)**
- **GIDDY (M 15)**
- **LUCIA (F 11)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE THREE: AT JD'S</u>**

- **NINA (F 35)**
- **LUKA (M 40's)**
- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE FOUR: AT GIDDY'S.</u>**

- **ZILPAH ( F 35)**
- **NINA (F 35)**
- **LUKA (M 40'S)**
- **GIDDY (M 15).**
- **JD (M 15)**

- **NARRATOR (M 30)**

**<u>SCENE FIVE: IN THE CITY.</u>**

- **NARRATOR (M 30)**
- **UNCLE BARRY (M 35)**
- **MRS. MWANGI (F 55) / LANDLADY**

**<u>INTRO:</u>**

**1. SFX: RESTAURANT AMBIENCE. CUTLERY.**

**2. NARRATOR:**

**(Speaking with a full mouth)** Oh, Hujambo na kwa mara nyingine karibu katika mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Bado ni wakati wa chakula cha mchana. Na kwa wale ambao ndio mwanzo wanajiunga nasi, Jina langu ni Gideon Leboo, afisa anayesimamia masuala ya mikopo, na mhusika mkuu katika mfululizo wa mchezo huu kuhusu "Starehe ya Kuazima- tatizo la kulipa mkopo" Kama mlivyosikia wakati wa sehemu ya kwanza ya mchezo huu, wakati nilikuwa shuleni na rafiki zangu, darasa letu lilikuwa na wanafunzi watukutu ,wenye kupenda kupiga makelele na vichekesho na ambalo lilipendwa sana na wanafunzi hasa wa rika la miaka 15

.Hata hivyo siku hiyo asubuhi, ingawa vichekesho vilikuwa vimezidi, tulimkosa sana rafiki yetu JD ambaye wanafunzi wengi walipenda sana kumcharia. JD si mtu wa kukasirika haraka na tangu ahusike kwenye ajali na baiskeli yake kuharibika, hajafika shuleni.

**<u>SCENE ONE: JD SKIVES OFF CLASS.</u>**

**3. SFX:** **CLASSROOM AMBIENCE:**

**4. STUDENT 1: (JOKING)** Babake Lenny ni mrefu hadi apige magoti ndipo aweze kuingia nyumbani.

**5. SFX:** **THE CLASS BURSTS OUT IN LAUGHTER.**

***KW BEGIN***

**6. STUDENT 2:** Ana Babako ni mfupi, mpaka wakati wa visa vya ufyatulianaji risasi vinapotokea, si lazima alale chini kujikinga risasi.

**7. SFX:** **LAUGHTER AND BOOS!**

**8. STUDENT 3:** Na wewe ni mweusi , kila mahali unapokwenda lazima upige makelele watu wakusikie ndipo wakupishe kwa sababu huonekana !

**9. STUDENTS: LAUGH**

***KW END***

**10. TEACHER MANDO:** Sawa, kila mmoja sasa akae mahali pake!

**11. SFX:** **DESKS PULLED, SHUFFLE OF FEET AS THE STUDENTS SETTLE DOWN.**

**12. TEACHER:** Asanteni. Na hakika mliweza kufurahia likizo yenu, sivyo? Sasa fungueni vitabu ukurasa wa.. …

**13. WINNIE:** **(Cuts in)** Ndio kila mmoja alifurahia isipokuwa JD.

**14. TEACHER:** **(Reprimanding)** Winnie, kwa nini unanikatiza! Unapasa kuinua mkono kama una jambo lolote la kusema! Sasa kuna mtu ana jambo la kusema? **( Pause)** Ndio Winnie nakuona umenyosha mkono!

**15. WINNIE:** JD hayuko darasani mwalimu Mando.

**16. TEACHER:** Nani anayefahamu kwanini JD hakufika shuleni?

**17. SFX:** **SILENCE.**

**18. TEACHER:** Giddy? Jenny?

**19. GIDDY/JENNY:** Hapana sijui mwalimu.

**20. TEACHER:** Nyinyi wawili jioni mkirudi nyumbani mwende nyumbani kwao kumjulia hali. Sawa! Tunaweza kuendelea sasa.

**21. SFX:** **PAPERS RUFFLE AS CHILDREN TURN PAGES. FADE OUT.**

**22. NARRATOR:**

Kila mmoja wetu pamoja na mwalimu Mando alifikiri JD ni mgonjwa nyumbani, kumbe tulikuwa tunakosema. JD alikuwa akizurura tu kuhangaika akitafuta pesa za kulipa deni la baiskeli yake ambayo aliichukua kwa mkopo. Maskini JD hangeweza kwenda shuleni kwa kuogopa kuchekelewa na wanafunzi wenzake baada ya kupoteza baiskeli yake mpya.

**SCENE TWO: AT GIDDY'S**

**23. SFX:** **NIGHT SOUNDS AS PEBBLES HIT WINDOW.**

**24. JD:** **(Calls almost whispering)** Psst! Psst! Giddy! Giddy!

**25. SFX:** **WINDOW OPENS.**

**26. JD:** **(Shouted whisper)** Ni mimi , Giddy tafadhali nifungulie..

***KW BEGIN***

**27. GIDDY:** **(Normal voice)** JD?! Unafanya nini usiku huu hapo nje?

**28. JD:** Shh! Usizungumze kwa sauti. Nifungulie kisha nitakueleza.

**29. GIDDY:** Sawa, wacha nikufungulie mlango.

**30. JD:** **(Panicky)** Hata usisumbuke nitapitia dirishani. Sitaki mama na dadako Lucia wajue niko hapa.

***KW END***

**31. GIDDY:** **(Hesitantly)** Sawa JD, wacha nikusaidie, nyosha mkono kwa hapa dirishani .

**32. SFX:** **FOOTSTEPS, CLIMBS THROUGH THE WINDOW.**

33. **JD:** **(Shivering)** Afadhali sasa hapa ndani, huko nje kuna baridi sana!

34. **GIDDY:** Ehhe, JD una tatizo gani? Umekuwa wapi siku zote? Na kwanini bado umevaa sare za shule na vitabu wakati huu? Na hata hukuwa shuleni leo!

35. **JD:** Nahitaji msaada wako shoga yangu! Kumekuwa usiku sana na siwezi kurudi nyumbani! Wacha nilale hapa kisha kesho nitaenda nyumbani.

36. **GIDDY:** Si sawa, ni sawa , lakini usinifiche jambo lolote. Mimi ni rafiki yako!

37. **SFX:** **KNOCKING ON THE DOOR**

38. **LUCIA:** **(Off mike)** Giddy! Unaongea na nani?

39. **GIDDY:** **(Whispers to JD)** Haraka upesi! Nenda ukajifiche chini ya kitanda! **(Shouts to Lucia)** Usiingie hapa chumbani kwangu Lucia!

Nasoma

40. **LUCIA:** **(Laughs as she sings)** Giddy anaongea peke yako! Giddy anajiongelesha!

**41. NARRATOR:**

JD anapata afueni baada ya Lucia kuondoka! Nikaenda kumuibia rafiki yangu chakula kilichokuwa kimebaki jikoni. Kilichonishangaza ni jinsi, alivyokibugia kana kwamba alikuwa hajala kwa siku kadhaa! Sasa angeweza kulala na kuamkia shida zake asubuhi ! Shida ambazo kwa hakika hazingepata ufumbuzi usiku huo!

**SCENE THREE: AT JD'S HOUSE.**

| | |
|---|---|
| **42. SFX:** | **NIGHT SOUNDS. KNOCK ON THE DOOR.** |
| **43. NINA:** | **(To herself)** Nadhani huyo ni JD. Lazima atueleze anatoka wapi usiku huu! |
| **44. SFX:** | **FOOTSTEPS, DOOR OPEN.** |
| **45. NINA:** | **(Angrily)** JD, Ni saa ngapi unafika nyumbani?... **(realises it is not JD)** Luka? Samahani mume wangu, nilidhani ni JD!. |
| **46. LUKA:** | JD? Unasema nini? Unamaanisha JD hajafika nyumbani saa hizi? |

**47. NINA:** Hajafika! Nilifikiri mko naye pamoja. Ndio sababu sikuwa na wasi wasi wa kumtafuta. **(Worried)** Sasa amechelewa wapi? Zinakaribia saa nne usiku!

**48. LUKA:** Twende ndani tukamsubiri.

**49. NINA:** Mtoto wako ametoweka na unasema twende ndani tukamsubiri?

**50. LUKA:** Usiwe na hofu! Mtoto wako amekuwa mtu mzima sasa! Tumsubiri kwa muda wa saa moja na nusu hivi na ikiwa bado hajafika basi tutaenda kumtafuta!

**51. SFX:** **DOOR CLOSES**

**52. NARRATOR:**

Lakini baada ya kusuburi kwa muda wa saa moja, JD hakufika, na hivyo wakaondoka moja kwa moja kwenda kumtafuta. Kwanza walifika nyumbani kwa kina Jenny, kisha baadaye nyumbani kwangu. Tayari tulikuwa tumelala! Na ghafla tukaamshwa na sauti ya mlango ukibishwa hodi. **SCENE FOUR: AT GIDDY'S.**

**53. SFX:** **NIGHT SOUNDS, PEOPLE SNORING**

**FOOTSTEPS, KNOCK ON THE DOOR**

**54. ZILPAH:** **(Scared)** Ni nani?

**55. NINA:** **(Off mike)** Nifungulie, Zilpah. Ni mimi Nina.

**56. ZILPAH:** Nina!

**57. SFX:** **FOOTSTEPS, DOOR OPEN.**

**58. ZILPAH:** Pita ndani Nina .. Oh, Luka, pia wewe uko hapa. Lakini ni usiku sana, kuna shida gani?

**59. LUKA:** Tunamtafuta mtoto wetu JD, amefika hapa?

**60. ZILPAH:** JD? Hapana, lakini subiri nimuulize Giddy **(Calls)** Giddy! Gideon!

**61. NARRATION:**

Mambo yalikuwa yamemharibika JD, sio tu rafiki yangu JD ambaye alikuwa mashakani bali mimi pia! Na nilihitaji ufumbuzi wa haraka kwa tatizo hili.

**62. ZILPAH:** **(from far)** Umemuona rafiki yako JD. Wazazi wake wako hapa wanamtafuta!

**63. GIDDY:** **(Whispers)** JD! JD! Amka haraka, wazazi wako wamefika… wako hapa!!

**64. ZILPAH:** **(from far)** Unafanya nini huko?

**65. GIDDY:** **(loud)** Sifanyi kitu mama.

**66. ZILPAH:** **(from far)** Gideon Leboo Mwanjala. Nimekuuliza swali. Umemuona JD? Kwani ni lazima ningie chumbani?

**67. GIDDY:** **(loud)** Hapana mma Sijamuona! **(To JD, whispering)** Haraka ruka nje kupita dirishani kabla mma hajaingia chumbani!

**68. JD:** **(Confused)** Lakini nitaenda wapi usiku huu?

**69.GIDDY:** Mimi sijui! Kimbia haraka nyumbani kwenu, ili wazazi wako wakirudi wakukute huko. Kisha utawaambia ulikuwa umechelewa ukifanya kazi za shule. Nenda haraka!

**70.JD**: Kwanini nisijifiche chini ya kitanda hapa chumbani kwako?

**71. GIDDY:** **(Whisper)** Mimi namfahamu sana mamangu. Akiingia hapa chumbani ,atapekua kila mahali. Kwa hivyo bora uondoke. Nenda..!Nenda..!

**72. SFX:** **SOMEONE JUMPS OUT WINDOW AND HITS GROUND.**

**73. SFX:** **FOOTSTEPS AS GIDDY’S MOTHER WALKS TO HIS BEDROOM.**

**74. SFX:** **DOOR OPENS.**

**75. ZILPAH:** WUlikuwa ukizungumza na nani Gideon?

**76. GIDDY:** Hakuna mtu yoyote mama.

**77. ZILPAH:** Una hakika hakuna mtu hapa ndani?

**78. SFX:** **MOVEMEMENTS AS SHE SEARCHES THE ROOM**

**79. GIDDY:** **(Pretending to be offended)** Sasa maaama! Si lazima upekue kila mahali chumbani mwangu. Nimekwambia hakuna mtu hapa ndani! Kwani huniamini?

**80. ZILPAH:** **(Ignores him)** Wazazi wa JD walikuwa hapa wakimtafuta hawajui amepitia wapi baada ya shule.

**81. GIDDY:** Mama.. mimi sijui.

**82. NARRATOR:**

Baadaye wazazi wa JD waliondoka wasijue wapi tena pa kwenda kumtafuta mtoto wao JD. Lakini walishangaa waliporudi nyumbani kumkuta JD akiwa amelala kitandani mwake. Anasema amekuwa darasani akisoma na wala hakuona muda ulivyokuwa unakwenda na ndio sababu ya kufika nyumbani kuchelewa. (**laughs**) JD ni kijana anayeweza kutunga sana.

Lakini unapozungumzia watu watukutu, tayari nimemgusia kuhusu mjombangu Barry, ambaye alikuwa mcheshi sana. Bado unamkumbuka? Mamangu anasema kuwa mjomba Barnabas alikuwa na tabia ya utukutu tangu utotoni .Yeye alipenda sana kuishi maisha ya kifahari. Alikuwa mtu mwenye kupenda starehe. Na kila wakati alipenda kuandamana na watoto wenye maisha ya juu shuleni. Lakini maisha haya yalimtatiza kwani aliiga tu maisha asiyoweza kumudu. Mara nyingi alijikuta akiomba au kucheza kamari, na kuanza tabia ya udanganyifu sio tu kwa rafiki zake bali hata kwa wale wadeni wake. Tabia hii pia ilimtawala na mjombangu. Alikuwa mtu maskini aliyeishi katika chumba kidogo cha kukodisha cha ukubwa wa mita kumi mraba,

lakini daima alikuwa akijigamba kwamba anaishi katika mitaa ya kifahari. (**laughs**).

**SCENE FIVE: IN THE CITY**

**83. SFX: NIGHT SOUNDS OUTSIDE, LOUD KNOCK ON THE DOOR.**

**84. LANDLADY:** Barnabas! Barnabas! Fungua mlango!

**85. SFX: SILENCE**

**86. LANDLADY:** Najua uko ndani! Fungua mlango! Nimekusikia ukiingia chumbani kupitia dirishani kama mwizi, najua uko ndani fungua mlango!

**87. BARRY: (Inside, snores loudly pretending to be asleep.)**

**88. LANDLADY: (Shouting)** Hutaki kufungua? subiri, sasa sina jinsi ila kumuuliza mtoto wangu avunje mlango. Na usijaribu kuruka kupitia dirishani maana utakutana na mtoto wangu mwengine hapo nje!

**89. SFX: FOOTSTEPS APPROACH, DOOR OPENS.**

**90. BARRY: (Yawning in pretence)** Bi. Mwangi, samahani sana nilikuwa usingizini! **(crawls)** Lakini umependeza usiku wa leo!

91. **LANDLADY:** Unafikrii mimi ni mjinga? Huyu mjinga anayesimama hapa anataka kodi yake sasa hivi!

92. **BARRY:** Hakuna shida Bi. Mwangi. Nitakulipa kodi yako hata ukitaka ya mwaka mzima!

93. **LANDLADY: (Laughs)** Wewe? Unilipe kodi ya mwaka mzima! Mimi si wale unaowadanganya!

94. **BARRY:** **(Convincingly)** Ni kweli Bi Mwangi! Nasubiri hundi ya pesa nyngi sana. Itakuwa tayari katika muda wa wiki mbili zijazo.

95. **LANDLADY:** Pia mwezi uliopita ulisema hayo hayo!

96. **BARRY:** Ni kweli, nakumbuka! Kulitokea kasoro kidogo wakati wa kutiwa sahihi katika hundi hiyo, lakini sasa tatizo hilo limerekebishwa.

97. **LANDLADY: (Decisively)** Siwezi kukuamini! Umenidanganya kwa muda mrefu sana. Hebu toka nyumbani mwangu!

98. **BARRY:** **(Desperate)** Basi wacha nilale usiku wa leo tu kesho nitahama asubuhi na mapema!

99. **LANDLADY:** Eeeeh... Ili kesho uweze kunidanganya tena? Sitaki!

100. **BARRY:** Lakini nitaenda wapi usiku huu Bi. Mwangi?

**101. LANDLADY:** Sitaki kujua! Toka nyumbani kwangu! Toka, toka!

**102. BARRY:** Bi. Mwangi nakuomba tafadhali....

**103. LANDLADY: (Finality)** Toka nje haraka..!

**104. BARRY:** Tafadhali nipe muda kidogo basi nipange mizigo yangu kwanza.

**105. LANDLADY:** Hapana! Utapanga mizigo yako baada ya kunilipa! Toka nje haraka! Nataka kufunga mlango wa nyumba yangu!

**106. SFX: FOOTSTEPS, PADLOCK. DOOR LOCKED.**

**OUTRO:**

**105. NARRATOR:**

Mjombangu ambaye ni mjanja sana, janja zake hazikuweza kumsaidia. Hakufahamu kwamba Bi. Mwangi alikuwa mjanja zaidi na tayari alikuwa ametambua janja zake ! (Sighs) Oh, Mungu wangu saa zimekwenda sana.

**106. SFX: CUP PLACED ON TABLE**

**107. NARRATOR:**

Hadi hapo sasa umefika ule wakati wa kurudi ofisini kabla ya mkubwa wangu kuanza kunibishia. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki unaweza kufanya hivyo kupitia mtandao wetu wa dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!